**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA FEDHA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**

PPRA
Public Procurement Regulatory Author

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. FB.192/247/01/B/142** **1 Novemba, 2024**

**Kwa Taasisi Nunuzi Zote na Wadau wa Ununuzi wa Umma:**

Yah: **KALENDA YA MAFUNZO YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA UNUNUZI WA UMMA (NeST) NA SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA YA MWAKA 2023 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2024**

Somo: **Mabadiliko ya maudhui na tarehe za mafunzo**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Serikali imetengeneza Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) ambao ulianza kutumika kuanzia mwezi Julai, 2023. Aidha, Sheria Mpya Na. 10 ya Mwaka 2023 na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 imeanza kutumika tarehe 17 Juni, 2024 na Kanuni zimeanza kutumika tarehe 1 Julai, 2024.

3. Hivyo, PPRA iliandaa Kalenda ya Mafunzo ya mwaka ambayo ilianza kutumika Mwezi Agosti, 2024. Kwa barua hii, Mamlaka inatangaza mabadiliko kadhaa kwenye ratiba ya mafunzo kutokana na mahitaji ya watumiaji na mabadiliko haya yameonyeshwa kwenye ratiba iliyoambatishwa.

4. Mafunzo ya pamoja ya kutumia mfumo yatatolewa kwa muda wa siku tano (5) kwa Taasisi Nunuzi na siku moja (1) kwa Wazabuni; na mafunzo ya Sheria, Kanuni pamoja na Uandaaji wa Nyaraka za Zabuni ndani ya mfumo yatatolewa kwa muda wa siku nne (4). Ada kwa kila mshiriki kutoka Taasisi Nunuzi ni **TZS 600,000.00;** na **TZS 100,000.00** kwa kila mshiriki kutoka kwa Wazabuni.

5. Maafisa Masuuli wanahimizwa kushiriki mafunzo haya na kuwaruhusu watumishi wao kuhudhuria mafunzo watakayochagua kushiriki kwa mujibu wa Kalenda ya Mafunzo iliyoambatishwa pamoja na mwaliko huu, ambayo pia inapatikana katika tovuti ya PPRA kupitia www.ppra.go.tz na mfumo wa mafunzo unaopatikana kupitia https://tsms.ppra.go.tz.

6. Ili kushiriki mafunzo, kila mshiriki anapaswa kujisajili katika mfumo wa mafunzo (https://tsms.ppra.go.tz), kisha kuchagua mafunzo anayotaka kushiriki na kuthibitisha

*3 Barabara ya Ununuzi, S. L. P 2865, 41104 TAMBUKARELI Dodoma, TANZANIA*
*Simu: +255 26 2963854, Barua Pepe: dg@ppra.go.tz, Tovuti: www.ppra.go.tz*

ushiriki kwa kulipia ada ya mafunzo kupitia Namba ya Malipo (Control Number) inayotolewa na mfumo wa mafunzo (tsms). Iwapo unahitaji Namba ya Malipo ya pamoja kwa washiriki zaidi ya mmoja, tafadhali wasilisha maombi kupitia barua pepe dg@ppra.go.tz.

7. Tunashukuru kwa ushirikiano wenu.

Dennis K. Simba
**MKURUGENZI MKUU**